



SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA
MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY (MBM) KATIKA
BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA**

2011/2012

JULAI, 2011

**HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA
MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY (MBM)
KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA
MWAKA WA FEDHA
2011/2012**

UTANGULIZI

- 1. Mhe. Spika**, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kujadili na hatimaye kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2011/2012.
- 2. Mhe. Spika**, kwanza ni wajibu wetu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwingi wa rehima kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena hapa leo hii ili kuendelea kujadiliana kuhusu shughuli muhimu za kimaendeleo katika nchi yetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie hekima, busara na atuongoze vyema ili tuweze kufanikisha majukumu yetu vizuri.

- 3. Mhe. Spika,** baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Ali Mohammed Shein kwa kupata ridhaa ya wananchi wa Zanzibar kuwaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo kufuatia ushindi alioupata baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba, 2010. Aidha, naomba pia kumpongeza kwa juhudi zake anazochukuwa katika kuendeleza umoja, utulivu na maelewano miongoni mwa Wazanzibari chini ya Serikali yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa. Bila shaka haya ni matunda ya kazi nzuri ya kujenga misingi ya maelewano iliyofanywa na mtangulizi wake Mhe. Dr. Amani Abeid Karume kwa upande mmoja na Mheshimiwa Seif Shariff Hamad kwa upande mwingine. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe Dr. Amani Abeid Karume kila la kheri katika maisha yake baada ya kukamilisha muda wake wa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.
- 4. Mhe. Spika,** nachukuwa nafasi hii pia kwa pamoja kuwapongeza Mheshimiwa Seif Shariff Hamad kwa kuteuliwa kwake kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Mh. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kuwa Makamo wa Pili wa Rais. Kwa hakika uteuzi wao umeanza kujenga matumaini makubwa miongoni mwa wananchi kutokana na

juhuri wanazochukuwa katika kutatua kero za wananchi.

5. **Mhe. Spika**, vile vile napenda kutoa pongezi za dhati kwako wewe Mh. Spika kwa kuchaguliwa kuliongoza Baraza letu tukufu kwa mara nyingine tena. Kwa hakika kuchaguliwa kwako kunaonesha ni kwa kiasi gani Waheshimiwa Wawakilishi wetu walivyo na imani juu ya utendaji wako wa kazi.

6. **Mhe. Spika**, Pongezi za pekee nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ali Abdalla Ali kwa jinsi walivyoanza kutushauri na kutuelekeza. Naomba nikiri kwamba michango yao imeisaidia sana Wizara katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi hiki kifupi.

7. **Mhe. Spika**, naomba kuwapongeza waheshimiwa Wawakilishi wote wa kuchaguliwa na wa kuteuliwa kwa kuingia katika Baraza hili tukufu. Naomba pia nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Mgogoni kwa kuniamini tena kwa kipindi chengine cha miaka mitano. Hakika imani yao kwangu ndio iliyokiwezesha chama changu cha CUF kunipendekeza kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa

Baraza la Mapinduzi katika nafasi ya Uwaziri. Hivyo, nachukua fursa hii kwanza kukishukuru chama changu kwa kunipendekeza, lakini zaidi kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuiteua kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Ninamhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa nitaitumikia nafasi hiyo kwa bidii na uadilifu mkubwa. Aidha nawaomba wananchi wa Jimbo la Mgogoni kuwa wastahamilivu kwa kutokuwa nao mara kwa mara jimboni kutokana na shughuli nyengine za kiserikali nilizokabidhiwa. Ninawaahidi kuwa tutazidi kuendelea kushirikiana katika kuleta maendeleo.

8. **Mhe. Spika**, sina budi kutoa mkono wa pole kwa familia ya aliyekuwa Afisa Mdamini wa Wizara ya Katiba na Sheria, Marehemu Hemed Rashid Kombo, aliyefariki tarehe 22 Machi 2011. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahala pema peponi, Amin.

9. **Mhe. Spika**, upatikanaji wa haki, kama unavyoelezwa katika Hotuba ya Uzinduzi wa Baraza jipya la Wawakilishi, ni nguzo muhimu inayosimamiwa na kutekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria. Katika Wizara ya Katiba na Sheria vyombo mbali mbali vinahusika na suala la usimamizi na utoaji wa haki vikiwemo Mahkama, Afisi ya Mkurugenzi Mashtaka, Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Katika miaka mitano ijayo,

Wizara ya Katiba na Sheria inakusudia kuimarisha usimamizi wa Sheria, utendaji wa vyombo vya sheria, uwezo wa utendaji na miundo mbinu ya taasisi hizo hasa kutoa umuhimu katika utekelezaji wa malengo ya jumla ya Wizara kama yalivyoainishwa mwishoni mwa hotuba hii.

10. **Mhe. Spika**, hivi sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imo katika hatua ya kuandaa utaratibu wa kupatikana kwa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano. Mhe. Spika, kama tunavyoelewa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetokana na muungano wa nchi mbili huru, na moja ya msingi wa muungano huo ni Mkataba wa Muungano ambao ndio uliophelekea kuwepo kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Hivyo, Katiba ya Jamhuri ya Muungano imetokana na makubaliano ya nchi mbili zilizounda muungano wetu.
11. **Mhe. Spika**, kwa msingi huo napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba Wizara ya Katiba na Sheria inachukuwa na itaendelea kuchukua hatua zinazopaswa ili kuhakikisha kwamba Zanzibar inashirikishwa na inashiriki ipasavyo hatua zote za kuandaa Katiba mpya.
12. **Mhe. Spika**, uwekaji wa utaratibu ni hatua moja lakini uandaaji wa Katiba yenyewe ni hatua ya pili. Katika hatua ya kwanza kunaandaliwa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Tume ya

kukusanya Maoni ya Wananchi kuhusu Katiba mpya. Katika hatua ya pili kutaandaliwa rasimu ya Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano. Katika hatua zote hizo Wizara itaendelea kuhakikisha kwamba maslahi ya Zanzibar yanalindwa inavyostahiki. Naamini kwamba sote tumejifunza hasara ya upande mmoja kutokushirikishwa katika jambo lenye maslahi kwa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Waswahili wanasema lililopita si ndwele tugange lijalo.

UPATIKANAJI WA FEDHA

13. Mhe. Spika, katika mwaka 2010/11 Wizara ilidhinishiwa Shilingi 4,242,443,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,299,543,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 1,942,899,000.00 kwa matumizi mengineyo. Fedha halisi zilizopatikana hadi Machi ni Shilingi 3,080,700,182.00 (73%). Kati ya hizo, Shilingi 1,774,647,245.00 (77%) ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 1,306,052,937.00 (67%) ni kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa kazi za maendeleo, fedha zilizoidhinishwa ni Shilingi 4,895,024,000.00 ambapo mchango wa Serikali ni Shilingi 1,325,000,000.00 na msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo ni Shilingi

3,570,024,000.00. Fedha za maendeleo zilizopatikana ni Shilingi 2,764,133,935.00 ambapo Shilingi 1,240,000,000.00 (94%) zilitoka Mfuko wa serikali na shilingi 1,524,133,935.00 (43%) zilitoka kwa wadau wa maendeleo. Wizara pia ilikadiria kukusanya Shilingi 296,250,000.00 ambapo hadi Machi 2011, fedha zilizokusanywa ni Shilingi 205,168,272.00 (69%) (viambatanisho vya 1, 2 & 3 vinahusika).

14. **Mhe. Spika**, hata hivyo Wizara ya Katiba na Sheria imepunguziwa Shilingi 87,200,000.00 kutoka katika bajeti yake ya mwaka 2010/2011 ili kuchangia bajeti ya Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hali hii imeathiri utendaji hasa katika kipindi hiki cha kumalizia mwaka wa fedha.
15. **Mhe. Spika**, maelezo zaidi ya utekelezaji wa kazi za kawaida na malengo kupitia idara na taasisi za Wizara kwa mwaka 2010/2011 ni kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

16. **Mhe. Spika**, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa shughuli za kila siku za Idara na Taasisi za Wizara. Idara hii ndio

kiungo baina ya Wizara na taasisi zake pamoja na Wizara nyengine.

17. Mhe. Spika, kufuatia muundo mpya wa Wizara na Idara za Serikali, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inayo majukumu yafuatayo:-

- kuandaa na kuratibu mipango ya Wizara ya muda mrefu, muda wa kati na mfupi, kutayarisha na kuwasilisha taarifa za utekelezaji, na kuandaa na kuratibu miradi ya maendeleo ya Wizara;
- kutayarisha Sera za Wizara; kusimamia utekelezaji wa sera hizo na sera mbalimbali za Kitaifa katika maeneo yanayoigusa Wizara ya Katiba na Sheria, na kutoa taarifa za sera mbalimbali za Serikali kwa Taasisi za Wizara;
- kuainisha, kuratibu na kufanya tafiti zinazohusiana na Wizara ya Katiba na Sheria na kutoa taarifa; kushirikiana na sekta nyengine za Serikali na zisizo za Kiserikali katika tafiti zinazohusiana na Wizara ya Katiba na Sheria; na

- kuweka na kuusimamia Mfumo wa Ufuatiliaji, Tathmini na utoaji taarifa; kufanya uchambuzi wa taarifa zote zinazohusu Wizara na Taasisi zake na kuzisambaza kwa matumizi.

18. Mhe. Spika, Ripoti ya Mapitio ya Wizara pamoja na utekelezaji wa sera kwa kipindi cha miaka 10 ilitayarishwa na kuwasilishwa katika Tume ya Mipango na katika iliyokuwa Afisi ya Waziri Kiongozi. Vile vile Idara imeshiriki katika kazi, mikutano na warsha mbalimbali zilizoandaliwa na Wizara nyengine ikiwemo Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo; Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Biashara; Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, n.k. Idara imeratibu kazi ya kutayarisha taarifa mbalimbali zikiwemo Ripoti ya Wizara kuhusu majukumu na muundo iliyowasilishwa Afisi ya Rais Ikulu, ripoti za Kamati za Baraza la Wawakilishi, matayarisho ya Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF), pamoja na Matayarisho ya Hotuba ya Bajeti.

19. Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti itatekeleza malengo yake kama yafuatayo:-

- i. Kuandaa Sera ya Sekta ya Sheria na Mpango Mkakati wa Wizara;
- ii. Kuratibu utayarishaji wa Mkakati wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria;
- iii. Kujenga mfumo wa usimamizi na uratibu wa taarifa muhimu za sekta ya sheria (*Information Management System*); na
- iv. Kuratibu utayarishaji Mikakati na tafiti za Idara na Taasisi za Wizara ukiwemo Mkakati wa kutekeleza Sera ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali.

20. Mhe. Spika, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza majukumu na malengo yake iliyojipangia kwa ufanisi katika mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha Jumla ya Shilingi 74,554,000.00 kwa kazi za kawaida na Shilingi 50,000,000.00 kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

21. Mhe. Spika, Idara ya Utumishi na Uendeshaji ni idara mpya katika Wizara ya Katiba na Sheria kufuatia muundo mpya wa taasisi za Serikali. Kabla muundo huu, majukumu ya Idara hii yalikuwa yakitekelezwa na iliyokuwa Idara ya Mipango na Sera. Idara ya Utumishi na Uendeshaji ni kiungo muhimu baina ya idara na taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara na taasisi nyengine na ina majukumu ya:-

- Kujenga mfumo wa usimamizi na uratibu wa taarifa muhimu za utawala na uendeshaji ndani ya Wizara;
- kusimamia na kuratibu utekelezaji shughuli zote za utumishi ndani ya wizara;
- kusimamia utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za wizara; na
- kuratibu shughuli za uendeshaji.

22. Mhe. Spika, Idara imeratibu na kukamilisha zoezi la kujaza dodoso la kuweka taarifa za raslimali-watu na mishahara. Kazi nyengine zilizoratibiwa na Idara ni pamoja na uhamaji wa Afisi ya Mrajis

Mkuu wa Serikali na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kutoka jengo la Mambo Msiige na kuhamia katika jengo la iliyokuwa Benki ya Watu wa Zanzibar lililopo Forodhani. Uhamiaji huu ni wa muda tu hadi hapo Wizara itakapokamilisha ujenzi wa jengo lake.

23. **Mhe. Spika**, Idara imeendelea kulifanyia matengenezo jengo la Wizara ili kuimarisha mazingira ya kazi. Aidha, Idara imeratibu hatua za awali za ujenzi wa jengo la Wizara litakalokuwepo Mazizini ambapo hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kuipata kampuni itakayotayarisha michoro na baadaye kusimamia ujenzi.
24. **Mhe. Spika**, Idara imesimamia vikao vya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji, Kamati ya Ukaguzi wa Ndani, na Vikao vya Bodi ya Zabuni.
25. **Mhe. Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, iliyokuwa Idara ya Mipango na Sera iliidhinishiwa Shilingi 475,880,000.00, kati ya fedha hizo jumla ya Shilingi 218,359,000.00 ni kwa mishahara na maposho na Shilingi 257,521,000.00 ni kwa matumizi mengineyo. Katika kipindi cha hadi mwezi Machi 2011, fedha zilizopatikana ni Shilingi 328,655,825.00 kati ya

hizo Shilingi 165,008,105.00 (76%) kwa ajili ya mishahara na maposho na Shilingi 163,647,720.00 (64%) ni kwa matumizi mengineyo (*kiambatanisho nam. 1 kinahusika*).

26. Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Idara ya Utumishi na Uendeshaji imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

- i. Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma kwa upande wa wizara na taasisi zake;
- ii. Kusimamia hatua ya pili ya ujenzi wa jengo jipya la wizara; na
- iii. Kuanzisha mifumo ya kuratibu na kusimamia shughuli za asasi za Kiraia.

27. Mhe. Spika, katika utekelezaji wa lengo la kusimamia ujenzi wa jengo jipya la wizara, jumla ya Shilingi 2,500,000,000.00 zimetengwa katika kifungu cha Programu Maalum ya Ujenzi wa Afisi za Serikali kilicho chini ya Afisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

- 28.** Mhe. Spika, ili Idara ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake naomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi 438,552,000.00 kwa kazi za kawaida.

MAHKAMA

- 29. Mhe. Spika,** Mahkama ni miongoni mwa nguzo tatu za dola. Jukumu kubwa la Mahkama ni kulinda na kusimamia haki za wananchi kwa kufuata Katiba na sheria za nchi ili kuhakikisha amani na utulivu unakuwepo nchini kwa madhumuni ya kukuza Utawala Bora. Katika miaka mitano ijayo, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria itatilia mkazo uimarishaji wa Mahkama katika maeneo yote matatu ya kitaasisi, taratibu za kiutendaji na uwezo wa wafanyakazi.
- 30. Mhe. Spika;** katika mwaka huu wa fedha, Mahkama ilipata mabadiliko makubwa ya uongozi wa juu. Mheshimiwa Jaji Hamid Mahmoud ambaye aliitumikia Mahkama akiwa Jaji Mkuu kwa miaka 22 alistaafu na nafasi hiyo kuteuliwa Mheshimiwa Jaji Omar Othman Makungu. Nampongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Jaji Hamid kwa utumishi wake. Aliitumikia Mahkama katika kipindi kigumu cha uhaba wa

watendaji na nyenzo. Namtakia maisha ya furaha baada ya kustaafu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Jaji Makungu kwa kuteuliwa. Naamini uzoefu, umahiri na uadilifu wake katika kusimamia haki utasaidia sana kuleta mageuzi na maendeleo katika Mahkama.

31. **Mhe. Spika**, Mahkama Zanzibar imegawika katika ngazi tano ikianza na Mahkama ya Mwanzo, Wilaya, Mkoa, Mahkama Kuu hadi ngazi ya juu ambayo ni Mahkama ya Rufaa ya Tanzania. Utaratibu huu ni wa kawaida ulimwenguni ili kutoa fursa kwa wananchi kutetea haki zao kikamilifu.

32. **Mhe. Spika**, pamoja na Mahkama hizo pia kuna Mahkama ya Kadhi wa Wilaya na Mahkama ya Kadhi Mkuu ambazo husikiliza mashauri ya kesi za kiislamu katika masuala yanayohusika na ndoa, talaka, mirathi, na matunzo ya watoto, iwapo wahusika wote ni waislamu. Sambamba na Mahkama hizo kuna Divisheni ya Mahkama ya Kazi chini ya Mahkama Kuu ambayo inashughulikia mashauri yanayohusiana na migogoro ya kikazi kati ya waajiri na waajiriwa. Mahkama katika shughuli zake za kila siku inavyo vitengo vya Mipango na Sera, Utawala na Uendeshaji, Mafunzo, Fedha, Sehemu ya Jinai, Madai, na Mahkama ya Rufaa.

- 33. Mhe. Spika,** katika kipindi cha Julai 2010 hadi kufikia mwezi Machi 2011, jumla ya kesi 8,371 zilifunguliwa katika Mahkama mbalimbali Unguja na Pemba ambapo zilizotolewa uamuzi ni 4714, ambazo ni sawa na asilimia 58. Katika kipindi kama hiki kwa mwaka uliopita zilifunguliwa kesi 5,472, ambapo kesi 2,195 sawa na asilimia 40 zilitolewa uamuzi. Katika kesi zilizofunguliwa, kesi 1392 ni za madai na 6681 ni za jinai (*angalia viambatanisho 6a & b*).
- 34. Mhe. Spika,** katika juhudi za kuimarisha miundombinu, matengenezo ya jengo la Mahkama Kuu Vuga yamefikia asilimia 50 na yanategemewa kuendelea katika mwaka ujao wa fedha. Aidha, Mahkama ya Mkoani Pemba imefanyiwa matengenezo na kwa upande wa Mahkama ya Mwanzo Chwaka matengenezo yanaendelea. Kwa upande mwingine, taratibu za kuanzisha Mahkama ya Biashara zinaendelea ambapo mtaalamu wa usimamizi wa kazi hiyo tayari ameteuliwa na sasa zipo katika hatua ya kufunga mkataba baada ya kupata ridhaa kutoka Benki ya Dunia ambao ndio wafadhili wa Mradi huu.

35. Mhe. Spika, katika kipindi hiki Majaji wanne na Mahakimu saba waliteuliwa ambapo Mahakimu wawili ni wa Mkoa na watano ni wa Mahkama ya Wilaya, kwa lengo la kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi na kupunguza mrundikano wa kesi. Aidha, Mahkama za Unguja na Pemba zimepatiwa vifaa vya kufanyia kazi na hivi sasa karibu nusu ya Mahkama za Zanzibar zinatumia kompyuta na kurahisisha kazi za uchapaji na upatikanaji wa kumbukumbu za kesi. Ni mategemeo yetu kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha 2011/2012 Mahkama zote za Zanzibar zitakuwa zinatumia kompyuta katika shughuli zake za kila siku. Katika kipindi hichi Mahkama imesomesha wafanyakazi wake katika mafunzo ya muda mrefu kama inavyooneshwa katika *kiambatanisho nam. 10b*.

36. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Mahkama ilitengewa Shilingi 1,391,000,000.00 kwa kazi za kawaida ambapo Shilingi 973,000,000.00 zilikadiriwa kutumika kwa mishahara na maposho na Shilingi 418,000,000.00 kwa matumizi mengine. Jumla ya fedha zilizopatikana ni Shilingi 1,009,947,568.00, zikiwemo Shilingi 722,161,387.00 (74%) za mishahara na maposho na Shilingi 287,786,181.00 (69%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, Mahkama iliidhinishiwa Shilingi

1,561,125,000.00 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi 550,000,000.00 ni kutoka Serikalini na Shilingi 1,011,125,000.00 kutoka kwa Wadau wa Maendeleo. Fedha zilizopatikana ni Shilingi 484,042,500.00 ambapo Shilingi 468,000,000.00 (85%) zilitoka serikalini na Shilingi 16,042,500.00 (2%) zilitoka kwa Wadau wa Maendeleo. Shilingi 38,000,000.00 zilikadiriwa kukusanywa katika kuchangia mapato ya Serikalini ambapo makusanyo halisi hadi kufikia mwezi Machi 2011 ni 71,609,832.00 (188%) *(viambatanisho 1, 2 & 3 vinahusika)*.

- 37. Mhe. Spika,** Mahkama bado inakabiliwa na ufinyu wa nafasi za afisi, uhaba na uchakavu wa majengo yake, mishahara midogo kwa mahakimu na upungufu wa wafanyakazi.
- 38. Mhe. Spika,** katika mwaka 2011/2012 Mahkama imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:
- i. Kuendelea na matengenezo ya jengo la Mahkama Kuu Vuga;
 - ii. Kuendelea na hatua za kuanzisha Mahkama ya Biashara;

- iii. Kuifanyia mapitio Sheria ya Mahkama ya Kadhi;
- iv. Kuandaa utaratibu wa kumpeleka Jaji Mkaazi Pemba; na
- v. Kuzikusanya pamoja hukumu za Mahkama Kuu kuanzia mwaka 2000 mpaka 2010 kwa matayarisho ya kuziweka katika "*Zanzibar Law Reports*".

39. Mhe. Spika, ili Mahkama iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka 2011/2012 naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 1,324,000,000.00 kwa kazi za kawaida na Shilingi 1,689,696,480.00 kwa kazi za maendeleo (zikiwemo Shilingi 300,000,000.00 kutoka serikalini). Aidha, Mahkama katika mwaka ujao wa fedha inakadiria kuchangia katika Hazina ya Serikali mapato ya Shilingi 48,000,000.00.

AFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

40. Mhe. Spika, Afisi ya Mwanasheria Mkuu ndio mshauri mkuu wa Sheria wa Serikali. Katika

kutekeleza jukumu hilo inafanya shughuli mbali mbali za kisheria. Miongoni mwa kazi hizo ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa taasisi mbali mbali za Serikali, uandishi wa Miswada, kusimamia kesi na mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali, kuandaa hati na nyaraka mbali mbali za kisheria na kufanya mambo mengine ya kisheria kwa niaba ya Serikali.

41. **Mhe. Spika**, majukumu niliyoyataja hapo juu bila shaka ni nyeti na muhimu sana. Ili kuyatekeleza Afisi inahitaji iwe imara kitaasisi na kiutendaji. Hivyo, katika miaka mitano ijayo, Serikali inakusudia kuiimarisha Afisi hii ili iweze kukabiliana ipasavyo na changamoto zilioko mbele yetu. Miongoni mwa yanayokusudiwa kutekelezwa ni pamoja na kuongeza idadi ya Wanasheria wa Afisi hii hadi kufikia mara mbili ya waliopo sasa, kuimarisha miundo mbinu ya Afisi katika majengo, vifaa na nyenzo, kuimarisha uwezo na taaluma za watendaji na kurekebisha muundo wa Afisi ili uweze kuleta ufanisi zaidi wa kazi. Aidha, katika kukabiliana na tatizo kubwa la uandaaji na usimamizi wa mikataba, Serikali imo katika hatua za kuanzisha kitengo maalum cha usimamizi wa mikataba chini ya Afisi hii.
42. **Mhe. Spika**, kama ilivyo kwa Mahkama, Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepata kiongozi mpya. Naomba kuchukua fursa hii kumpongeza

Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

43. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imeendelea kutekeleza shughuli za kawaida, ambapo miswada saba iliandikwa na kuwasilishwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Miongoni mwa Miswada hiyo ni ule wa Sheria ya Marekebisho ya Kumi ya Katiba ya Zanzibar. Afisi ilitayarisha matangazo ya kisheria 98 na tayari yameshawasilishwa kwa Mpiga chapa Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Kati ya matangazo hayo, kuna sheria ndogondogo nane. Vile vile Afisi imesimamia kesi 59 za Madai ambapo kesi tatu kati ya hizo ni mpya na 56 ni kesi za zamani ambazo zimekuwa zikiendelezwa (*angalia kiambatanisho nam. 7*).

44. Mhe. Spika, Afisi kupitia mradi wa BEST imewapatia Wanasheria na Maafisa wengine wa Sheria kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali, Mashirika, na Taasisi Binafsi mafunzo yanayohusiana na Sheria za Biashara na Mikataba. Aidha, imenunua vitabu vya Sheria kwa ajili ya matumizi ya Maktaba ya Afisi. Afisi pia imeendelea kutoa taarifa zake mbalimbali kwa kutumia tovuti yake yenye anuani www.agc.go.tz.

Kwa kutumia nafasi hii, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi wote pamoja na wananchi kwa ujumla kuitumia tovuti hii ili kupata taarifa juu ya Sheria zetu na mambo mengine ya kisheria kwa ujumla.

45. Mhe. Spika, Afisi imekamilisha uchapishaji wa sheria za Zanzibar kuanzia mwaka 1980 hadi mwaka 2010 ambapo jumla ya "Volume" 15 zimechapishwa na kusambazwa kwa wadau. Sheria za mwaka 2011 bado zipo kwa Mchapaji kwa hatua za mwisho. Aidha, Afisi imechapisha nakala zisizopungua 3,000 za Katiba ya Zanzibar na kuzisambaza kwa Taasisi mbalimbali za Serikali, Mashirika, na Taasisi binafsi. Hivi sasa Afisi inategemea kuchapisha nakala nyengine ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata Katiba. Aidha, kupitia msaada wa Programu ya Pamoja ya Mashirika ya Umoja wa Mataifa (JP5), Afisi hii imeshakamilisha tafsiri ya Katiba ya Zanzibar kwa lugha ya Kiingereza na kuchapisha nakala 450.

46. Mhe. Spika, napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa hivi sasa Wizara kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu inashiriki vyema katika utaratibu wa maandalizi ya Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo

vikao vinne vya pamoja vimefanyika. Kwa kupitia vikao hivyo, mambo yaliyoonekana kuwa na utatanishi katika rasimu ya mwanzo ya Mswada wa Sheria ya Tume ya Kuratibu Maoni ya Katiba, yalijadiliwa kwa kina na muafaka wa kuufanyia marekebisho katika maeneo yote ya msingi ulipatikana. Inatarajiwa baada ya hatua za kiserikali kukamilika, Mswada huo utapelekwa Bungeni na kupitishwa kuwa Sheria itayosimamia utaratibu wa kupata Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- 47. Mhe. Spika,** ni nia ya Wizara ya Katiba na Sheria kwamba baada ya kumaliza hatua ndogo ndogo za kisheria zinazoendelea, na baada ya kuliarifu Baraza la Mapinduzi, tutafanya utaratibu maalum kwa Waheshimiwa Wawakilishi na Wananchi kuwaelezea namna hoja zilizotolewa na Wazanzibari zilivyozingatiwa na kuingizwa katika rasimu mpya ya Mswada wa Utaratibu wa kuanzisha Katiba mpya.
- 48. Mhe. Spika,** Afisi imewasomesha wafanyakazi wake watano katika ngazi mbalimbali kama inavyooneshwa katika kiambatanisho nam. 10b. Aidha, Afisi imefanya matengenezo sehemu ya maktaba na mategenezo madogo madogo ya Afisi kwa ujumla. Hivi sasa, Afisi imo katika hatua

za awali za ujenzi wa jengo lake jipya, Mazizini Unguja.

49. Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ya Mwanasheria Mkuu iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 546,000,000.00 zikiwemo Shilingi 161,088,000.00 za mishahara na maposho, na Shilingi 384,912,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana ni Shilingi 403,408,103.00 ambapo Shilingi 139,093,103.00 (86%) ni kwa mishahara na maposho na Shilingi 264,315,000.00 (69%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, Jumla ya Shilingi 1,718,899,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambapo zilizotoka Serikalini ni Shilingi 250,000,000.00 na kwa wadau wamaendeleo ni Shilingi 1,468,899,000.00. Katika fedha za maendeleo zilizopatikana, Shilingi 245,000,000.00 (98%) zilitoka Serikalini na Shilingi 315,869,423.00 (22%) zilitoka kwa washirika wa maendeleo (*viambatanisho nam. 1&2 vinahusika*). Sababu kubwa ya kupungua fedha za wafadhili ni kutokana na kuchelewa kuanza kwa Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Uchumi na Fedha unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

50. Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Afisi ya Mwanasheria Mkuu imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:

- i. Kufanya marekebisho ya muundo na mfumo wa utendaji wa Afisi;
- ii. Kuendeleza awamu ya mwanzo ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Afisi;
- iii. Kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mikataba ya Serikali; na
- iv. Kuziweka Pamoja (*Consolidation*) na Kuzichapisha Sheria za Zanzibar za 1959 hadi 2010 ambazo zitajumuisha Sheria zote.

51. Mhe. Spika, ili kuiwezesha Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 612,077,000.00 kwa kazi za kawaida na shilingi 1,576,329,000.00 kwa kazi za maendeleo.

TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

52. Mhe. Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kipindi chote tokea ilipoanzishwa imekuwa chini ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Tume hii imekaa kipindi kirefu bila ya kutekeleza majukumu yake kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo ya kukosekana kwa Mwenyekiti, Katibu na Watendaji wengine. Katika mwaka huu wa fedha, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alimteua Katibu. Hivi sasa Tume inaendelea kujipanga kwa kuongeza watendaji (wanasheria). Watendaji hao ndio watakuwa na jukumu la kufanya utafiti juu ya sheria mbalimbali zinazohitaji kufanyiwa mapitio kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Tume. Aidha, Makamishna wanatarajiwa kuteuliwa katika kipindi hichi cha 2011/2012 ili kazi zake zianze rasmi.

53. Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema hapo awali, Tume ya Kurekebisha Sheria ilikuwa ni sehemu ndani ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Moja kati ya malengo ya Wizara ilikuwa ni kuiondoa Tume kwenye Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili iwe inajitegemea na kuweza kupanga mikakati yake kikamilifu na kutekeleza kwa ufanisi. Ninayo furaha kulijulisha rasmi Baraza lako tukufu kuwa Wizara imefanikiwa kutekeleza lengo hilo kwani Afisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo imeipatia

Tume ya Kurekebisha Sheria Fungu lake nam. 46. Hatua hii itatuwezesha kuikuza na kuipa hadhi inayostahiki.

54. Mhe. Spika, Tume imefanikiwa kupata sehemu katika jengo la Eacrotanal, na ilihamia rasmi mwezi wa Mei, mwaka 2011. Aidha, Watendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ambapo wafanyakazi wawili wamesoma Shahada ya Uzamili ya Sheria.

55. Mhe. Spika, katika mwaka 2011/2012, Tume ya Kurekebisha Sheria imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:

- i. Kuimarisha Afisi ya Tume na kuifanya iwe na hadhi kwa mujibu wa kazi zake;
- ii. Kuweka muundo na mfumo imara wa utendaji wa Afisi;
- iii. kuongeza idadi ya Wanasheria na watendaji wengine wa Afisi na kuendelea kuimarisha uwezo na taaluma zao;
- iv. Kuzipitia Sheria ya Watu wenye Ulemavu Nam. 9 ya mwaka 2006, Sheria ya

Ushahidi Nam. 5 ya mwaka 1917, na Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Nam. 16 ya mwaka 1986; na

- v. Kuanzisha na kuimarisha mashirikiano na jumuiya mbali mbali zenye majukumu sawa na ya Tume.

56. Mhe. Spika, ili kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 174,914,000.00 kwa kazi za kawaida.

AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

57. Mhe. Spika, Kifungu cha 56A cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kimetaja kuwepo kwa Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na mamlaka yake kiutendaji. Sambamba na hilo, Sheria Nam. 2 ya mwaka 2010, chini ya kifungu cha 4(1), nayo imeanzisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na kuonesha utawala na majukumu yake kiutendaji. Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ina mamlaka ya kusimamia na kuendesha kesi zote za jinai katika Mahkama zote za kiraia za Zanzibar.

- 58. Mhe. Spika**, hadi kufikia mwezi wa Machi 2011 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 74, ambapo Pemba wapo 15 na Unguja 59 (*angalia kiambatanisho nam. 10a*).
- 59. Mhe. Spika**, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ilifungua na kusimamia jumla ya kesi 953 na kupokea majalada 204 kutoka Jeshi la Polisi kwa ajili ya kupatiwa ushauri kuhusiana na makosa mbalimbali (*angalia kiambatanisho nam. 6c*). Katika kuimarisha mfumo mzima wa upashanaji habari juu ya takwimu za mienendo ya kesi, Afisi imeanzisha "*Data base*" maalum inayotumika kwa ajili ya kutoa taarifa za kesi, aina na sehemu zinakotokea pamoja na muendelezo wake Mahakamani. Afisi imeendelea kuwapatia ushauri mbalimbali wananchi wanaofika Afisini kwa dhamira hiyo.
- 60. Mhe. Spika**, Afisi pia imeendelea na utoaji wa elimu kwa jamii kupitia semina, mafunzo mbalimbali kwa kupitia jarida lake la SHAHIDI. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 Afisi imetoa matoleo matatu ya Jarida la SHAHIDI kwa nakala 6,000. Aidha, Afisi imetoa mafunzo kwa vyombo vya ulinzi na taasisi nyengine kuhusu Haki za Binadamu, Serikali yenye Muundo wa

Umoja wa Kitaifa na Nafasi ya Vyombo vya Ulinzi katika Serikali yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa. Kwa upande mwingine, Afisi imeendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake katika ngazi tafauti kama inavyooneshwa katika *kiambatanisho nam. 10b*.

61. Mhe. Spika, lengo la kuendesha mashtaka katika Mahkama nne za wilaya limeendelea kushughulikiwa kwa kuzifikia wilaya za Mjini na Magharibi. Aidha, hatua kadhaa zimefikwa ili kujiandaa na kuzifikia wilaya nyengine ikiwemo kuwapatia wanasheria saba mafunzo ya vitendo ya uendeshaji kesi katika Mahkama mbalimbali huko Tanzania Bara na mikutano ya maandalizi kwa wadau wa jinai ngazi ya wilaya. Aidha, jengo la Afisi ya Uendeshaji Mashtaka Wilaya lililopo Mwanakwerekwe limekamilika na kuanza kutumika. Kwa upande wa Pemba, Afisi imekamilisha matengenezo ya Afisi ndogo ya waendesha mashtaka katika Mahkama ya Konde.

62. Mhe. Spika, Afisi imeendelea na matayarisho ya ujenzi wa jengo la afisi Pemba ambao unatarajiwa kuanza mwanzoni wa mwezi wa July 2011. Vile vile Afisi imeendelea na ujenzi wa jengo la makaazi Pemba ambalo limefikia hatua ya kuezekwa. Aidha, jengo la kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria hapa Unguja limekamilika kwa asilimia 75. Kwa upande mwingine Maafisa

watatu wamefanya ziara ya mafunzo Arusha - Chuo cha Uongozi Afrika Mashariki na Kusini (ESAMI) na Mahkama ya Kimataifa ya Mauaji ya Halaiki Rwanda (ICTR), ikiwa ni moja kati ya hatua za matayarisho ya uanzishwaji wa Kituo hicho. Kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Afisi inatarajia mwanzoni mwa mwaka ujao wa fedha kuanza kupokea vifaa vya kutendea kazi, usafiri na malipo kwa ajili ya washauri wa kitaalamu juu ya mitaala ya kituo. Kituo hiki kitakuwa kinatoa huduma ndani na nje ya Zanzibar.

- 63. Mhe. Spika**, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliidhinishiwa Shilingi 719,000,000.00 kwa kazi za kawaida ambapo Shilingi 339,000,000.00 zilikadiriwa kwa mishahara na maposho na Shilingi 380,000,000.00 kwa Matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2011, Afisi imeingiziwa Shilingi 498,005,501.00 zikiwemo Shilingi 274,122,726.00 (81%) kwa mishahara na maposho na Shilingi 223,882,775.00 (59%) kwa matumizi mengineyo. Aidha Shilingi 750,000,000.00 ziliidhinishwa kwa kazi za maendeleo, kati ya fedha hizi Shilingi 500,000,000.00 ni kutoka katika mfuko wa serikali na Shs 250,000,000.00 ni mchango wa washirika wa maendeleo. Fedha zilizopatikana ni Shilingi

772,000,000.00 ambapo Shilingi 420,000,000.00 (84%) zilitoka Serikalini na Shilingi 352,222,012.00 (141%) kutoka kwa wafadhili. *(viambatanisho nam. 1&2 vinahusika).*

64. Mhe. Spika, bado suala la kuondosha waendesha mashtaka wa Jeshi la Polisi katika mahkama zote linakwamishwa na ufinyu wa bajeti. Aidha, uhaba wa miundombinu ya afisi unaleta ugumu wa kiutendaji ambapo Afisi ya Mkurugenzi Mashtaka inahitaji kuwa na ofisi angalau katika kila mkoa. Suala hili tutajitahidi kulitekeleza kwa awamu katika kipindi hichi cha 2011/2012.

65. Mhe. Spika, kwa mwaka ujao wa fedha 2011/2012, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imejipangia malengo yafuatayo;

- i. Kupeleka waendesha mashtaka katika wilaya nyengine zilizobaki;
- ii. Kuimarisha na kuendeleza uwezo wa Afisi kiutendaji, taratibu za uendeshaji kazi na rasilimali watu;
- iii. Kuimarisha miundombinu ya Afisi kwa kukamilisha ujenzi wa nyumba ya kuishi

Chake Chake na kujenga Afisi ndogo ya Waendesha Mashtaka katika Mahkama Kuu, Chake Chake; na

iv. Kuanza kazi kwa Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria.

66. Mhe. Spika, ili Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iweze kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo yake kwa mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 724,000,000.00 kwa kazi za kawaida, Shilingi 534,000,000.00 kwa kazi za maendeleo (zikiwemo Shilingi 250,000,000.00 kutoka Serikalini), na ruzuku ya Shilingi 50,000,000.00 kwa ajili ya Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria.

AFISI YA MUFTI WA ZANZIBAR

67. Mhe. Spika, Afisi ya Mufti wa Zanzibar ina jukumu kubwa la kutoa miongozo na kutatua migogoro mbalimbali ya Kidini kwa wananchi wa Zanzibar.

68. Mhe. Spika, Afisi imeendelea kutekeleza kazi za kawaida kwa kushughulikia migogoro mbalimbali

ambayo imepelekwa Afisini hapo kwa kupatiwa ufumbuzi. Migogoro 13 kati ya 15 iliyowasilishwa Afisini hapo imepatiwa ufumbuzi wakati migogoro miwili ya misikiti inaendelea kufanyiwa kazi. Afisi imeendelea kuelimisha jamii juu ya kuepuka migogoro kwa kutumia hotuba za Ijumaa misikitini Unguja na Pemba. Aidha, Afisi ilijikita katika mawaidha na mihadhara juu ya Amani na Utulivu kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 na baada ya uchaguzi kwa kuwapeleka Maulamaa katika Majimbo yote ya Uchaguzi ya Zanzibar. Vile vile Afisi iliratibu dua ya pamoja kuiombea nchi amani kuelekea Uchaguzi Mkuu.

- 69. Mhe. Spika,** Afisi imefikisha misaada mbalimbali ya kijamii kwa watoto yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu katika shehia za Fumba, Chukwani, Mombasa na Tomondo Wilaya ya Magharibi Unguja. Vile vile ilifanya mikutano mitatu ya mafunzo ya elimu ya Ukimwi kwa Walimu wa madrasa za watoto na watu wazima na pia Maimamu wa Misikiti ya Ijumaa kwa Wilaya ya Magharibi Unguja. Aidha, katika mwaka wa fedha 2011/2012 afisi inatarajia kufanya mikutano na kutoa misaada katika Wilaya za Wete na Micheweni Pemba. Wilaya zilizobakia misaada itatolewa kwa kadri hali itakavyoruhusu.

70. Mhe. Spika, Afisi imeendelea kupokea maswali mbalimbali kutoka kwa wananchi ndani na nje ya nchi. Katika kipindi hicho maswali 120 yaliulizwa na waumini wa hapa Visiwani na nje na yote yamejibiwa. Vile vile Afisi imepokea Masheikh wawili kutoka nchini Misri na Iran kwa ajili ya kusoma Qur-an katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani; na ujumbe wa watu wanne kutoka Saudia kwa ajili ya kufuatilia ujenzi wa Msikiti Mkuu Zanzibar kama ni zawadi kutoka kwa Mfalme Abdalla wa Saudi Arabia. Vile vile afisi ilipokea ujumbe wa Jumuiya ya Kiislamu ya Uturuki.

71. Mhe. Spika, Afisi ya Mufti imeendelea kuwasomesha wafanyakazi wake, ambapo mfanyakazi wake mmoja aliyekuwa akisomea ngazi ya udaktari (PhD) amemaliza masomo yake na kuripoti kazini. Watendaji wengine waliopo masomoni ni kama inavyoonekana katika *kiambatanisho nam. 10b.*

72. Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ya Mufti wa Zanzibar iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 159,239,000.00. Kati ya fedha hizo Shilingi 93,563,000.00 ni kwa mishahara na maposho, na Shilingi 65,676,000.00 kwa matumizi mengineyo. Hadi

kufikia Machi, 2011 fedha zilizopatikana ni Shilingi 108,866,751.00. Kati ya hizo Shilingi 65,510,751.00 (70%) ni kwa mishahara na maposho, na Shilingi 43,356,000.00 (66%) kwa matumizi mengineyo (*kiambatanisho nam. 1 kinahusika*).

73. Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha 2011/2012, Afisi ya Mufti imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- i. Kuimarisha uratibu wa taasisi za kidini;
- ii. Kuanzisha huduma za maktaba ya kiislam;
- iii. Kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Afisi; na
- iv. Kuanzisha kituo cha kuhifadhi kumbukumbu za maulamaa wa Zanzibar.

74. Mhe. Spika, ili Afisi ya Mufti wa Zanzibar iweze kutekeleza kikamilifu malengo iliyojiwekea kwa mwaka ujao wa fedha 2011/2012, naliomba

Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 140,435,000.00 kwa kazi za kawaida.

AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI

- 75. Mhe. Spika,** Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011. Afisi ya Mrajis wa Mkuu wa Serikali imeendelea kutekeleza kazi zake za kawaida za usajili. Hadi kufikia Machi, 2011 jumla ya vizazi 31,076 vimesajiliwa ambapo wanaume 19,421 na wanawake 11,655. Kwa upande wa vifo, jumla ya vifo 1,523 vimesajiliwa ambapo wanaume 897 na wanawake 626.
- 76. Mhe. Spika,** kampuni zilizosajiliwa ni 186, majina ya biashara (*Business names*) 300, alama za biashara (*Trademarks*) zilizosajiliwa ni 157 na Jumuiya zisizo za kiserikali (NGOs) 46. Nyaraka zilizosajiliwa ni 756 ambazo ni nyaraka za dhamana za Benki (A1), nyaraka za mauziano na urithi (A2), nyaraka za wakfu, hiba, kodi , kiapo na mikataba ya uhaulishaji wa vyombo vya moto (A3) na waraka wa kufuta dhamana za Benki (A4).
- 77. Mhe. Spika,** jumla ya ndoa zilizosajiliwa kupitia mashekhe ni 2,800 na talaka ni 225. Aidha ndoa

zilizosajiliwa mahakamani ni 125 na talaka 375.
(*angalia viambatanisho nam. 8a&b*).

78. Mhe. Spika, Afisi inashirikiana na Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka na Upatikanaji wa Takwimu ili kuleta ufanisi. Mradi huu una lengo la kukuzifanyia mapitio sheria tatu (*Sheria Nam. 10 ya Vizazi na Vifo ya mwaka 2006, Sheria ya Ndoa na Talaka kwa Waislamu Sura ya 91 na Sheria ya Ndoa na Talaka kwa Wasiokuwa Waislamu Sura ya 92 ya Sheria za Zanzibar*) zinazoongoza usajili pamoja na kutengeneza mfumo wa kisasa utakaotumia kompyuta. Hivi sasa tayari Mshauri Mwelekezi ameshawasilisha ripoti ya pili ambayo imejumuisha pia rasimu ya sheria mpya.

79. Mhe. Spika, Afisi imefanikiwa kukamilisha Sheria ya Usajili wa Mikataba ya Mali zinazohamishika na tayari imepitishwa na Baraza lako tukufu. Kwa upande mwingine, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko zimo katika kutekeleza mpango wa mapitio ya mfumo wa leseni za biashara Zanzibar hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza ya mapitio imekamili na tayari mtaalamu amewasilisha ripoti ya kazi hiyo. Ripoti hiyo imefanyiwa mapitio na Kamati ya Usimamizi ili kumwelekeza mtaalamu kuifanya bora zaidi.

Hatua nyengine za utekelezaji mpango huo zinaendelea.

- 80. Mhe. Spika,** katika kutekeleza lengo la kuzibadilisha nyaraka na kumbukumbu na kuziweka katika mfumo wa kielektroniki (digitization of papers records), Afisi tayari imeshatangaza zabuni kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, matangazo kwa ajili ya zabuni ya kazi ya upembuzi wa mahitaji ya Afisi yamekwishatolewa.
- 81. Mhe. Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 wafanyakazi wanne wamepelekwa masomoni. Miongoni mwao mmoja anasomea shahada ya kwanza, wawili stashahada na mmoja cheti (*angalia kiambatanisho nam. 10b*).
- 82. Mhe. Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 307,766,000.00, ambapo Shilingi 142,435,000.00 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na maposho na Shilingi 165,331,000.00 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2011 fedha zilizopatikana ni Shilingi 231,625,079.00 ambapo Shilingi 117,621,005.00 (72%) kwa ajili ya mishahara na maposho na Shilingi 114,004,074.00 (69%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, Jumla ya Shilingi 865,000,000.00

ziliidhinishwa na kupatikana kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambazo kati yake, Shilingi 25,000,000.00 zilitoka Serikalini na Shilingi 840,000,000.00 zilitoka kwa wadau wamaendeleo. Kwa upande wa mapato, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali katika mwaka wa fedha 2010/2011, ilikadiria kukusanya jumla ya Shilingi 258,250,000. Hadi kufikia Machi 2011, Shilingi 133,558,440.00 (52%) zilikusanywa (*viambatanisho vya 1, 2 & 3 vinahusika*).

83. Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali imedhamiria kutekeleza malengo yafuatayo:-

- i. Kuendelea kuifanyia marekebisho mifumo na sheria zinazoongoza usajili;
- ii. Kuimarisha Usimamizi na Usajili wa Tasnia ya Mali za Ubunifu;
- iii. Kurekebisha kasoro za kiutendaji zinazochelewesha upatikanaji wa vyeti na huduma nyenginezo; na

- iv. Kuimarisha mashirikiano na taaasisi zote zinazohusika na masuala ya usajili na kumbukumbu.

84. Mhe. Spika, ili kuiwezesha Afisi itekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 336,281,000.00 kwa kazi za kawaida na Shilingi 2,168,055,706.00 (zikiwemo Shilingi 90,000,000.00 kutoka Serikalini) kwa kazi za maendeleo. Aidha, Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali inakadiria kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali jumla ya Shilingi 263,415,000.00.

AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

85. Mhe. Spika, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar imedhamiria kutekeleza jukumu kubwa la kukusanya Mirabaha (fedha zinazokusanywa kwa watumiaji wa kazi za hakimiliki) kwa watumiaji wote. Dhamira hiyo inatekelezwa baada ya kuzingatia malalamiko ya watumiaji wa kazi za Hakimiliki kutokana na ukubwa wa viwango kwa kuvifanyia marekebisho mwezi Oktoba, 2010. Ufanisi wa utekelezaji wa shughuli hii

unategemea zaidi kuwa na idadi ya kutosha ya wafanyakazi pamoja na taaluma na mafunzo vitakavyoweza kuinua mwamko na mwitikio wa kufanya malipo kwa matumizi ya kibiashara. Aidha hali hii itapelekea wamiliki wa kazi kuikubali kikamilifu dhana ya usimamizi wa pamoja wa Hakimiliki.

- 86. Mhe. Spika,** Afisi imeendesha jumla ya vikao vitatu vya Bodi ya Hakimiliki ambavyo ndivyo vinavyotoa mwongozo katika utekelezaji wa shughuli za Afisi. Aidha Afisi kwa kushirikiana na Shirika la Milki Ubunifu Ulimwenguni (*World Intellectual Property Organization - WIPO*) imewapeleka mafunzoni maafisa wake wawili katika mafunzo ya usimamizi na utumiaji wa mfumo wa Kimataifa, *WIPO Software for Collective Management of Copyright and Related Rights (WIPOCOS)* wa kuhifadhi kumbukumbu za wabunifu na kazi zao huko Harare, Zimbabwe; na imeshiriki katika kikao cha tatu cha "*Subregional Technical Meeting on Harmonization of Copyright Legislations in Southern and Eastern Africa*". Kikao kimesaidia sana katika kutoa mwelekeo wa mabadiliko ya Sheria za Hakimiliki. Vile vile, Afisi imempeleka mfanyakazi mmoja katika mafunzo ya muda mrefu.

- 87. Mhe. Spika**, katika kuhakikisha ufanisi wa matumizi halali na ulipiaji wa hakimiliki, Afisi imezifanyia marekebisho kanuni za Utoaji wa Leseni na Ulipiaji mirabaha za mwaka 2009 kwa kupunguza viwango vya malipo. Marekebisho hayo yamezingatia malalamiko ya watumiaji kazi kibiashara. Kanuni mpya za Utoaji wa Leseni na Ugawaji wa Mirabaha zimeshatangazwa na kuanza kutumika.
- 88. Mhe. Spika**, katika kipindi hiki, kazi 64 za hakimiliki zilisajiliwa Unguja na Pemba. Idadi hiyo iliyosajiliwa inafanya jumla ya kazi zote za hakimiliki zilizosajiliwa kufikia 704 kuanzia mwaka 2007 kazi hiyo ilipoanza. Kwa uchambuzi wa kazi zilizosajiliwa (*angalia kiambatanisho nam. 8c*).
- 89. Mhe. Spika**, hadi kufikia mwezi Machi 2011 Afisi imetoa leseni tatu kwa matumizi halali ya kazi za hakimiliki katika kituo cha redio cha Zenj FM, Chuchu FM na Hits FM. Aidha, Afisi imetoa ushauri wa kisheria, kuandaa na kupitia mikataba ya wamiliki na watumiaji wa kazi za hakimiliki kibiashara. Vile vile uhamasishaji juu ya umuhimu wa kulipia hakimiliki umefanyika kwa kusambaza ankara za malipo kwa vituo vyote vya utangazaji vya hapa nchini kuwataka wafanye malipo.

90. Mhe. Spika, Afisi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na watengenezaji wa filamu Tanzania "*Steps Entertainment Ltd*", ilifanya msako mkali kwenye maduka yanayokodisha kazi za hakimiliki kwa ajili ya kukamata nakala zisizokuwa halali na vile vile kufuatilia iwapo wamiliki wa maduka hayo wamelipa katika Afisi ya Msajili wa Hakimiliki. Katika msako huo uliofanyika Agosti 28, 2010 nakala haramu 2,472 zilikamatwa zikijumuisha DVD 2027, CD 215, mikanda ya VHS 230 na magamba matupu ya VHS 38. Wale waliokamatwa katika msako huo walitakiwa kulipa fidia kwa wamiliki wa kazi za hakimiliki zilizohusika.

91. Mhe. Spika, vile vile Afisi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na Baraza la Manispaa iliendesha msako mwengine Septemba 27, 2010 na kukamata nakala 5,217 zisizo halali na wamiliki wanne wanaotuhumiwa kuuza kazi za hakimiliki kinyume na Sheria ya Hakimiliki (Sheria Nam. 14) ya mwaka 2003, walifunguliwa mashtaka. Hukumu ya kesi hiyo imetoka kwa kuwaachilia huru washtakiwa. Kwa kutoridhishwa na hukumu hiyo, Afisi kwa kushirikiana na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imekata rufaa katika Mahkama ya Mkoa Vuga.

- 92. Mhe. Spika,** katika kuhakikisha mwenendo mzuri wa kesi Afisi imefanya mafunzo kwa mahakimu na waendesha mashtaka wa mahkama za wilaya Unguja ambako kesi za uvunjaji wa hakimiliki zinasimamiwa. Mafunzo hayo yalifanyika Oktoba 9, 2010.
- 93. Mhe. Spika,** kuelimisha jamii ni lengo la muda mrefu la Afisi hasa kutokana na upya wa dhana ya Hakimiliki. Afisi kwa kushirikiana na Televisheni Zanzibar inaendesha vipindi vya kila wiki ambapo jumla ya vipindi 12 vya televisheni vilirushwa hewani. Aidha Afisi imeandaa vipeperushi vya kuelimisha jamii umuhimu wa leseni ya hakimiliki kibiashara na umuhimu wa kusajili kazi za hakimiliki.
- 94. Mhe. Spika,** Afisi inakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo ufinyu wa nafasi, ukosefu wa maktaba yenye vifaa maalum kwa ajili ya kuhifadhia mali za hakimiliki, usalama kwa watendaji wa hakimiliki, na maslahi hafifu kwa wataalamu.
- 95. Mhe. Spika,** katika mwaka wa fedha 2010 / 2011, Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar iliidhinishiwa ruzuku ya Shilingi 120,000,000.00.

Kati ya hizo, Shilingi 28,600,000.00 kwa mishahara na maposho na Shilingi 91,400,000.00 kwa matumizi mengine (*kiambatanisho nam. 1 kinahusika*).

96. Mhe. Spika, pamoja na kujiimarisha kiutendaji katika mwaka ujao wa fedha, Afisi imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

- i. Kuongeza kasi ya ulipiaji kazi za Hakimiliki kwa watumiaji kibiashara; na
- ii. Kuipitia na kuifanyia marekebisho Sheria ya Hakimiliki.

97. Mhe. Spika, ili Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar iweze kutekeleza majukumu na malengo yake katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha 2011/ 2012 naliomba Baraza lako tukufu liidhinisha Ruzuku ya Shilingi 100,000,000.00 kwa kazi za kawaida.

KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA

- 98. Mhe. Spika**, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ina wajibu wa kusimamia Mali za Wakfu, Amana, Mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Iddi Kitaifa, Hijja, Zakka na Misaada ya kheri. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Kamisheni imetekeleza kazi kama ifuatavyo:
- 99. Mhe. Spika**, Kamisheni imeendelea kutoa ushauri kwa wawekaji nyakfu ambao siku hizi wanazidi kuhamasika kwa kujiwekea *sadakatul jaariya* (sadaka yenye kuendelea). Hadi kufikia Machi 2011 jumla ya Shilingi 95,478,565.00 zilikusanywa ikiwa ni kodi za nyumba za Wakfu na Amana. Shilingi 19,942,000.00 zimetumika kwa kuzifanyia matengenezo nyumba nane.
- 100. Mhe. Spika**, inajulikana kuwa fedha hizi ni kidogo sana kwani kodi inayotozwa ni ndogo, wapangaji hawalipi, n.k. Pia inatambulika kuwa kuna wapangaji wakorofi ambao wanakodishwa kwa bei ndogo lakini wao wanakodisha (sublet) kwa bei kubwa sana bila ya idhini ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Matatizo haya yameonekana na kuanza kuchukuliwa hatua.
- 101. Mhe. Spika**, katika kuendeleza ujenzi wa nyumba ya Mbweni ambayo ni fidia ya mashamba yaliyokatwa eka, Shilingi 60,000,000.00

zimetumika kumalizia sehemu ya chini ya nyumba hiyo. Gharama za ujenzi huu zimetoka katika milki za wakfu wenyewe na mkopo. Juhudi zinachukuliwa ili kuutafutia mradi huu ufadhili au mkopo usio na riba ili ukamilike. Aidha, Kamisheni imeendelea kusimamia Mashamba manne na Vikataa tisa vya Wakfu na imeweza kukusanya Shilingi 800,000.00 kutokana na kodi. Mapato hayo yamegaiwa kwa wanufaika wa nyakfu hizo.

102. Mhe. Spika, Tirka 368 za mirathi zimefunguliwa na tirka 319 zenye thamani ya Shilingi 939,052,788.66 zimefungwa. Aidha tirka 136 bado zinaendelea kushughulikiwa. Aidha Kamisheni ilikabidhiwa fleti 78 za Jumba nam. 10 Michenzani zikiwa ni za wafidiwa waliofariki. Fleti 52 zenye thamani ya Shilingi 1,548,560,000.00 zimesharithishwa. Tirka za fleti saba zinaendelea kushughulikiwa. Jitihada zinafanywa ili kuwapata warathi wa fleti 19 zilizobaki na wasipopatikana taratibu za kuziweka Amana katika *baytulmaal* zitafanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji, na Nishati. Pia migogoro 21 imesuluhishwa, 16 inaendelea kutafutiwa ufumbuzi na zipo kesi 22 zinazoendelea katika mahkama mbalimbali.

103. Mhe. Spika, Kamisheni iliratibu safari ya Hija kwa Taasisi zote 17 za Tanzania ambapo tisa kati ya hizo zimesajiliwa Zanzibar. Jumla ya Mahujaji

2,181 kutoka Tanzania walitekeleza ibada ya Hijja. Mahujaji 1,141 kati yao walisafirishwa na Taasisi zilizosajiliwa Zanzibar (*angalia kiambatanisho nam. 9*). Kamisheni pia imeshaanza kuelimisha waumini ili waipe kipaumbele ibada ya Hijja hasa ukizingatia kuwa Tanzania ina fursa ya kupeleka mahujaji 30,000 lakini bado idadi hiyo hatujaikaribia. Matatizo makubwa kwa upande wa Hijja ni pamoja na ucheleweshaji wa Mahuhaji wakati wa kurudi. Wizara imejitahidi kuandaa mpango mzuri na wasafirishaji ili kuondoa usumbufu huo. Kwa upande mwingine, Kamisheni imepokea misaada ya nyama, tende, nguo, futari na kuigawa kwa yatima, masikini na wahitaji mjini na mashamba kwa Unguja na Pemba. Aidha Kamisheni imekuwa ikisimamia na kushirikiana na Jumuiya mbalimbali za misaada ya kheri kwa hapa Zanzibar.

104. Mhe. Spika, Zakka ni nyenzo muhimu katika kuondosha umasikini. Kamisheni imeshaandaa rasimu ya muongozo wa kuelimisha mambo mbalimbali yanayohusu shughuli za zakka ili ibada hiyo ifanywe kwa usahihi na kwa kuzingatia mahitaji ya wakati tulionao. Muongozo huo umeshaanza kutumiwa katika uelimishaji. Sambamba na hilo, Kamisheni imeunda timu ya washauri waelekezi ambao wamejitolea katika

kupendekeza utaratibu wa kuundwa Mamlaka ya Zakka. Wizara inaamini kwamba iwapo waamin watashajiishwa ipasavyo, Zakka itasaidia sana katika kupunguza umasikini hapa Zanzibar.

105. Mhe. Spika, utafiti kuhusu Kamisheni tokea kuasisiwa kwake na mikondo iliyopitia hadi kufikia sasa tayari umeshafanyika. Aidha baadhi ya watendaji wamepatiwa mafunzo mbalimbali yatakayoimarisha utendaji na ufanisi wa kazi. Hivyo, kazi ya kuweka mpango mkakati imeshajengewa misingi lakini bado haijakamilika. Mpango huo pia utaandaa mfumo mzima wa uwekaji na utunzaji nyaraka na kumbukumbu za Kamisheni kwa mujibu wa mahitaji ya zama tulizonazo.

106. Mhe. Spika. Katika kunyanyua viwango vya elimu na uzoefu wa wafanyakazi, wafanyakazi tisa wanaendelea na masomo na wafanyakazi watatu wamemaliza masomo na kurejea kazini. (*angalia kiambatanisho nam. 10b*).

107. Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Kamisheni iliidhinishiwa ruzuku ya Sh 300,000,000.00. Kati ya hizo, Shilingi 217,544,000.00 kwa mishahara na maposho na

Shilingi 82,456,000.00 kwa matumizi mengine
(*kiambatanisho nam. 1 kinahusika*).

108. Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana Kamisheni imebaini matatizo yafuatayo, na imeyawekea mikakati ya kuyatatua katika mwaka ujao wa fedha:

- Uvamizi na kutokujulikana baadhi ya mali za Wakfu zikiwemo nyumba, ardhi na mashamba;
- Ufinyu wa elimu katika jamii juu ya utoaji wa Zakka, makusudio ya sheria katika wakfu na masuala ya Mirathi;
- Madeni sugu na udanganyifu unaofanywa na wanaokodishwa mali za wakfu na amana, ambapo baadhi ya hatua tumeshaanza kuzichukua; na
- Nyenzo za kutendea kazi na mazingira ya utendaji bado yanahitaji kuwa mazuri zaidi.

109. Mhe. Spika, Katika mwaka ujao wa fedha 2011/2012, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- i. Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa mali za wakfu na amana ili kuongeza ufanisi, uhifadhi na mapato yake;
- ii. Kukamilisha mfumo wa shughuli za zakka; na
- iii. Kuwaendeleza watendaji na kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi

110. Mhe. Spika, Ili Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iweze kutekeleza majukumu na malengo yake katika kipindi cha 2011/2012 naliomba Baraza lako tukufu liidhinishhe Ruzuku ya Shilingi 300,000,000.

AFISI KUU PEMBA

111. Mhe. Spika, Afisi Kuu - Pemba ni kiungo kikuu katika kusimamia shughuli za utendaji wa Idara pamoja na Taasisi za Wizara kwa upande wa Pemba. Katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Afisi

Kuu - Pemba imeweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na imeendelea kusimamia na kuratibu maelekezo ya Wizara juu ya utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa ujumla. Aidha, katika kuwaendeleza wafanyakazi, Afisi imewapeleka katika masomo ya muda mrefu wafanyakazi saba (*angalia kiambatanisho 10b*).

112. Mhe. Spika, katika kuendeleza na kusimamia shughuli za kiislamu Afisi Kuu Pemba kupitia Afisi ya Naibu Mufti, ilipokea Maswali 75 ya kisheria yanayohusu migogoro ya ndoa, misikiti, mirathi na ya kifamilia ambayo yamepatiwa ufumbuzi kwa mujibu wa sheria za kiislam.

113. Mhe. Spika, Afisi Kuu - Pemba, ilikadiria kutumia Shilingi 223,558,000.00 kwa kazi za kawaida ambapo Shilingi 125,955,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na maposho na Shilingi 97,603,000.00 kwa matumizi mengineyo. Kiasi kilichopatikana ni Shilingi 178,727,048.00 ambapo Shilingi 106,582,756.00 (85%) ni mishahara na maposho na Shilingi 72,144,292.00 (74%) ni matumizi mengineyo (*kiambatanisho nam. 1 kinahusika*).

114. Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Afisi Kuu - Pemba inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

- i. Kuratibu maandalizi ya Sera ya Sekta ya Sheria na Mpango Mkakati wa Wizara;
- ii. Kuratibu utayarishaji wa Mkakati wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria;
- iii. Kuratibu utayarishaji Mikakati na tafiti za Idara na Taasisi za Wizara ukiwemo Mkakati wa kutekeleza Sera ya Jumuiya Zisizo za Kiserikali.
- iv. Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma; na
- v. Kujenga mfumo wa usimamizi na uratibu wa taarifa muhimu za sekta ya sheria (*Information Management System*).

115. Mhe. Spika, ili Afisi Kuu - Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kama ilivyotarajiwa, katika mwaka wa fedha 2011/2012 naomba

kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 282,178,000.00
kwa ajili ya kazi za kawaida.

MALENGO YA JUMLA YA WIZARA

116. Mhe. Spika, kwa mwaka ujao wa fedha, Wizara itaweka kipaumbele kwa kuhakikisha kuwa Zanzibar inashiriki ipasavyo kwenye utaratibu mzima wa matayarisho ya kuandaa na uandaaji wa Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Wizara inakusudia kutayarisha mkakati wa mageuzi katika sekta ya sheria na kuandaa sera ya sekta ya sheria.

117. Mhe. Spika, Wizara itaendelea kupambana na tatizo la ucheleweshaji wa kesi katika mahkama zetu na kuhakikisha matatizo ya wananchi katika usimamizi na ufuatiliaji wa haki zao yanapungua kwa kiasi kikubwa. Aidha, Wizara itaendeleza ushirikiano kwa kuwaelimisha zaidi watendaji wa wilayani na masheha ili kuhakikisha vyeti vya kutosha vinapatikana kwa wakati. Vile vile, Wizara itaendelea kushirikiana na Idara ya Uchapaji kuhakikisha upatikanaji wa nakala za kutosha za vyeti kwa wakati muafaka.

118. Mhe. Spika, pamoja na maelezo niliyoyatoa hapo juu, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, naomba kutoa kwa muhtasari mwelekeo wa malengo ya utekelezaji ambayo Wizara imedhamiria kuyatekeleza kama ifuatavyo:-

1. Kuongoza taratibu zote za uandaaji wa Katiba mpya ya Jamhuri ya muungano kwa upande wa Zanzibar;
2. Kukuza upatikanaji wa haki na kuzingatia Utawala wa Sheria;
3. Kutekeleza Mpango wa Pamoja wa Mageuzi wa Usimamizi wa Haki za Jinai Zanzibar (*Criminal Justice Reform Framework*);
4. Kutayarisha Mkakati wa Mapitio ya Sekta ya Sheria (*legal Sector Reform Strategy*);
5. Kufanyia mapitio sheria mbalimbali za Wizara zikiwemo Sheria ya Hakimiliki na Sheria ya Mahkama za Kadhi; na kutayarisha Sheria ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu na Sheria ya Afisi ya Mrajis Mkuu;

6. Kutekeleza Mpango wa Mageuzi katika Mifumo ya Usajili;
7. Kuimarisha Uwezo wa watendaji, vitendea kazi na kujenga mazingira bora zaidi ya kazi kwa Taasisi za Wizara; ikiwa ni pamoja na kuielimisha jamii juu ya Taasisi za Wizara;
8. Kuimarisha utendaji wa Baraza la Ulamaa chini ya Afisi ya Mufti wa Zanzibar;
9. Kutayarisha Mfumo wa Shughuli za Zakka;
10. Kujenga jengo la Afisi za Wizara, kujenga Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba na kuendelea na matengenezo ya jengo la Mahkama Kuu; na
11. Kuimarisha uratibu wa shughuli zote za Wizara na Taasisi zake.

SHUKURANI

119. Mhe. Spika, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuiwasilisha Hotuba hii

mbele ya Baraza lako tukufu. Aidha, haitokuwa jambo la busara kama sitatoa shukurani zangu za dhati kwa wale wote waliotoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za wizara yangu.

120. Mhe. Spika, shukurani maalum nazitoa kwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu. Vile vile, natoa shukurani kwa Watendaji Wakuu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa juhudi wanayoonesha na mashirikiano katika kutekeleza majukumu yao. Najua ni muda mfupi tokea kukabidhiwa jahazi hili lakini kwa ushirikiano uliopo naamini na tunamuomba Mwenyezi Mungu atufikishe salama salmini. Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Baraza hili kwa michango yao yenye manufaa kwa wizara na taifa kwa ujumla.

121. Mhe. Spika, Wizara imekuwa ikifanya kazi zake kwa mashirikiano na wafadhili na wahisani mbalimbali na kwa heshima na taadhima naomba ruhusa yako kuwashukuru wale wote wanaotusaidia wakiwemo UNDP, AfDB, WIPO, WTO, Shirika la Mali Bunifu la Afrika (ARIPO), Benki ya Dunia, Norway, Sweden, Africa Muslims Agency, Serikali ya Saud Arabia, Benki ya Maendeleo ya Kiislam (IDB), vikundi mbalimbali

vilivyosafirisha Mahujaji, na Jumuiya na Taasisi mbalimbali za kidini Zanzibar.

HITIMISHO

122. Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu wachangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na baadaye waidhinishe matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 ya jumla ya Shilingi 4,556,991,000.00 kwa kazi za kawaida na Shilingi 6,018,081,186.00 kwa kazi za maendeleo (zikiwemo 690,000,000.00 kutoka serikalini na Shilingi 5,328,081,186.00 kutoka kwa wadau wa maendeleo) ili iweze kutekeleza malengo yake iliyojipangia. Aidha, naliomba Baraza lako likubali mchango wa Shilingi 311,415,000.00 ikiwa ni mapato yanayokadiriwa kukusanywa na Wizara ya Katiba na Sheria, ambayo yataingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

123. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja

Kiambatanisho 1: Fedha Zilizolingizwa kwa Matumizi ya Kawaida

IDARA	FEDHA ZILIZODHINISHWA 2010/2011			JUMLA FEDHA ZILIZOINGIZWA A JUL 2010-MACH 2011	WAST ANI WA JUMLA (%)	MCHANGANUO WA FEDHA ZILIZOINGIZWA			
	JUMLA	MSHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO			MISHAHARA NA MAPOSHO	(%)	MATUMIZI MENGINEYO	(%)
14 – Mahkama	1,391,000,000	973,000,000	418,000,000	1,009,947,568	73%	722,161,387	74%	287,786,181.00	69%
15 - Afisi ya Mwanasheria Mkuu	546,000,000	161,088,000	384,912,000	403,408,103	74%	139,093,103	86%	264,315,000	69%
35 - Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	719,000,000	339,000,000	380,000,000	498,005,501	69%	274,122,726	81%	223,882,775	59%
36/04 - Idara ya Mipango, Sera na Uendeshaji	475,880,000	218,359,000	257,521,000	328,655,825	69%	165,008,105	76%	163,647,720	64%
36/05 - Afisi ya Mufti wa Zanzibar	159,239,000	93,563,000	65,676,000	108,866,751	68%	65,510,751	70%	43,356,000	66%
36/11 - Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali	307,766,000	142,435,000	165,331,000	231,425,079	75%	117,421,005	82%	114,004,074	69%
36/03 - Afisi Kuu Pemba	223,558,000	125,955,000	97,603,000	178,727,048	80%	106,582,756	85%	72,144,292	74%
Ruzuku - Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	300,000,000	217,544,000	82,456,000	231,464,307	77%	163,157,949	75%	68,306,358	83%
Ruzuku - Afisi ya Msimamizi wa Hakimiliki	120,000,000	28,600,000	91,400,000	90,000,000	75%	21,389,463	75%	68,610,537	75%
Jumla Vote 36	1,586,443,000	826,456,000	759,987,000	1,169,139,010	74%	639,070,029	84%	530,068,981	70%
JUMLA	4,242,443,000	2,299,544,000	1,942,899,000	3,080,700,182	73%	1,774,447,245	77%	1,306,052,937	67%

Kiambatanisho 2: Taarifa ya Fedha za Miradi Julai 2010 - Machi 2011

JINA LA MRADI	MAKISIO 2010/2011			FEDHA ZILIZOTOLEWA (JULAI 2010 – MACHI 2011)			ASILIMIA YA FEDHA ILIYOTOLEWA NA MAKISIO	
	SMZ	MUHISANI	JUMLA	SMZ	MUHISANI	JUMLA	SMZ	MHISANI
Mradi wa Kuimarisha Mahkama	550,000,000	1,011,125,000	1,561,125,000	468,000,000	16,042,500	484,042,500	85%	2%
Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu	250,000,000	1,468,899,000	1,718,899,000	245,000,000	315,869,423	560,869,423	98%	22%
Mradi wa Kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	500,000,000	250,000,000	750,000,000	420,000,000	352,222,012	772,222,012	84%	141%
Mpango wa Kurekebisha Mazingira ya biashara Zanzibar (Afisi ya Mraji Mkuu wa Serikali)	25,000,000	840,000,000	865,000,000	25,000,000	840,000,000	865,000,000	100%	100%
JUMLA KUU	1,325,000,000	3,570,024,000	4,895,024,000	1,240,000,000	1,524,133,935	2,764,133,935	94%	43%

Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato 2010/2011 na Makadirio ya 2011/2012

IDARA/TAASISI	MAKADIRIO 2010/2011	MAKUSANYO HALISI 2010/11	%	MATARAJIO JUNI 2011	JUMLA HADI JUNI 2011	%	MAKADIRIO 2011/2012
MRAJIS MKUU WA SERIKALI (36/11)	258,250,000	133,558,440	51.72	30,200,000	163,758,440	63	263,415,000
14 - MAHAKAMA	38,000,000	71,609,832	188.45	6,000,000	77,609,832	204	48,000,000
JUMLA KUU	296,250,000	205,168,272	69.26	36,200,000	241,368,272	81	311,415,000

Kimbatanisho 4: Makadirio ya Matumizi kwa Kazi za Kawaida na Maendeleo 2011/2012 (000)

FUNGU/IDARA	KAZI ZA KAWAIDA					KAZI ZA MAENDELEO			
	JUMLA	MSHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	UNGUJA	PEMBA	MCHANGO WA SERIKALI	WAHISANI	JUMLA FEDHA ZA MAENDELEO	JUMLA KUU
14 Mahkama	1,324,000	724,000	600,000	967,000	357,000	300,000	1,389,696	1,689,696	3,013,696
15 Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	612,077	137,216	474,861	612,077	-		1,576,329		2,188,406
35 Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	774,000	328,000	446,000	550,000	174,000	250,000	284,000	534,000	1,308,000
Tume ya Kurekebisha Sheria	174,914	59,457	115,457	174,914	-	-	-	-	174,914
36/04 Idara ya Mipango, Sera na Utafiri	74,554		74,554	74,554		50,000		50,000	124,554
36/06 Idara ya Utumishi na Uendeshaji	438,552	220,442	218,110	438,552					438,552
36/03 Afisi Kuu Pemba	282,178	182,006	100,172	-	282,178			0	282,178
36/05 Afisi ya Mufti wa Zanzibar	140,435	70,208	70,227	140,435	-			0	140,435
36/11 Afisi ya Mraji Mkuu wa Serikali	336,281	149,344	186,937	273,579	62,702	90,000	2,078,056	2,168,056	2,504,337
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (R)	50,000	15,000	35,000	50,000					50,000
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana (R)	300,000	217,544	82,456	229,950	70,050			0	300,000
Afisi ya Msajili wa Hakimiliki (R)	100,000	42,625	57,375	100,000				0	100,000
JUMLA VOTE 36	1,272,000	622,000	650,000	947,284	344,880	140,000	2,078,056	2,218,056	3,490,056
JUMLA KUU	4,606,991	2,145,842	2,461,149	3,631,175	945,930	690,000	5,328,081	6,018,081	10,625,072

Kiambatanisho 5: Miradi ya Maendeleo 2011 - 2012

Namba ya Mradi	Jina la Mradi	Mchango wa Serikali	Mchango wa Wahisani	Mhisani	Jumla Kuu
74017	Ujenzi wa Jengo la Wizara ya KS				
74018	Mapitio ya Sekta ya Sheria	50,000,000.00	-		50,000,000.00
72201	Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Makampuni na Kuimarisha Afisi	30,000,000.00	2,078,055,706.80	BEST	1,121,897,000.80
74019	Marekebisho ya Mfumo wa Usajili na Takwimu za Vizazi na Vifo na Ndoa na Talaka.	60,000,000.00			60,000,000.00
72212	Mradi wa kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	250,000,000.00	284,000,000.00	ADB/ UNDP	534,000,000.00
72234	Kuimarisha Mahkama Kuu	265,000,000.00			265,000,000.00
72239	Uanzishwaji wa Mahkama ya Biashara	35,000,000.00	1,389,696,480.00	BEST	1,424,696,480.00
72185	Kuimarisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu		1,576,329,000.00	BEST	1,576,329,000.00
	JUMLA KUU	690,000,000.00	5,328,081,186.80		6,018,081,186.80

Kiambatanisho 6a:Ufunguaji wa Kesi Mahakamani Julai 2010 hadi Machi 2011

Mahkama ya	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
	Madai			Jinai		Madai		Jinai	
	Jumla Zilizofunguliwa	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi
Rufaa	16	0	0	0	0	8	0	5	3
M/Kuu Vuga	166	43	8	25	10	31	8	7	4
M/Kuu Pemba	19	2	0	4	3	10	0	0	0
Kazi	10	10	0	0	0	0	0	0	0
Kadhi Mkuu	52	36	16	0	0	0	0	0	0
Kadhi Rufaa Pemba	16	0	0	0	0	10	6	0	0
Mkoa Vuga	251	36	1	186	16	3	0	6	3
Mkoa Mfenesini	185	3	0	92	76	0	0	9	5
Mkoa Mwera	183	3	0	131	41	1	0	5	2

Kiambatanisho 6a:Ufunguaji wa Kesi Mahakamani Julai 2010 hadi Machi 2011

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
	Madai			Jinai		Madai		Jinai	
Mahkama ya	Jumla Zilizofunguliwa	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi
Mkoa Wete	79	0	0	58	16	0	0	3	2
Mkoa Chake	48	9	0	25	11	3	0	0	0
Wilaya Mw/kwe	1212	53	8	839	310	0	0	1	1
Wilaya Mwera	258	4	0	176	77	1	0	0	0
Wilaya Mkokotoni	963	1	0	501	459	1	1	0	0
Wilaya Mfenesini	332	9	2	220	101	0	0	0	0
Wilaya Makunduchi	246	0	0	144	102	0	0	0	0
Wilaya Mkoani	59	0	0	41	16	0	0	1	1
Wilaya Chake	79	1	0	53	23	1	1	0	0
Wilaya Wete	127	0	0	82	44	1	0	0	0

Kiambatanisho 6a:Ufunguaji wa Kesi Mahakamani Julai 2010 hadi Machi 2011

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
	Madai			Jinai		Madai		Jinai	
Mahkama ya	Jumla Zilizofunguliwa	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi	Zilizofunguliwa	Zilizotolewa Uamuzi
Wilaya Konde	109	2	2	67	38	0	0	0	0
Watoto Vuga	12	0	0	10	2	0	0	0	0
Watoto Mwera	8	0	0	7	1	0	0	0	0
Watoto Mfenesini	8	0	0	8	0	0	0	0	0
Watoto Chake	5	0	0	5	0	0	0	0	0
Watoto Wete	0	0	0	0	0	0	0	0	0
Jumla	4413	212	37	2674	1346	70	16	37	21

Kiambatanisho 6b: Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Mwanzo na Kadhi

Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Mwanzo						Ufunguaji wa Kesi Mahkama za Kadhi		
Mahkama ya Mwanzo	Kesi za Madai			Kesi za Jinai		Mahkama za Kadhi Wilaya	Kesi za Madai	
	Jumla	Zilizo funguliwa	Zilizo tolewa uamuzi	Zilizo funguliwa	Zilizotolewa uamuzi		Zilizofunguliwa	Zilizotolewa uamuzi
Manispaa Malindi	616	-	-	616	582			
Mwanakwerekwe	193	46	12	147	73	Mjini	597	347
Mwera	315	9	2	306	199	Mwera	20	3
Makunduchi	130	19	3	111	20	Mfenesini	42	27
Chwaka	100	6	4	94	75	Mkokotoni	63	49
Mfenesini	236	3	0	233	217	Makunduchi	26	8
Mkokotoni	120	9	1	111	20	Chake chake	92	45
Mkoani	25	10	0	15	8	Mkoani	28	24
Kengeja	10	5	4	5	5	Kengeja	6	1
Chake chake	116	15	2	101	26	Chwaka	8	6
Wete	83	6	3	77	36	Wete	64	11
Konde	32	3	2	29	14	Konde	36	15
Jumla	1976	131	33	1845	1275	Jumla	982	536

Kiambatanisho 6c: Kesi zilizofunguliwa na kusimamiwa na DPP

Kesi Zilizofunguliwa na Kusimamiwa na Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Julai 2010 hadi Machi 2011	
MAHKAMA	IDADI YA KESI
MAHKAMA YA RUFAA TANZANIA	0
MAHKAMA KUU VUGA	32
MAHKAMA KUU PEMBA	21
MAHKAMA YA MKOA VUGA	185
MAHKAMA YA MKOA MWERA	96
MAHKAMA YA MKOA MFENESINI	38
MAHKAMA YA MKOA WETE	60
MAHKAMA YA MKOA CHAKE CHAKE	32
MAHKAMA WILAYA MWANAKWEREKWE	348
JUMLA	812

Kiambatanisho 7: Miswada na Machapisho - Afisi ya Mwanasheria Mkuu 2010/2011

a. Miswada ya Sheria iliyoandaliwa
i. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ardhi, 2010;
ii. Sheria ya Kondominion, 2010;
iii. Sheria ya kuweka Miundo, Uendeshaji na Usimamizi wa Utumishi wa Umma Zanzibar;
iv. Sheria ya Usajili wa Mikataba ya Mali Zinazohamishika na Mambo yanayohusiana nayo
v. Sheria wa Uendelezaji , Ukuzaji na Uwekaji wa viwango na Ubora wa Bidhaa na Usimamizi wa huduma zinazolingana na hizo; na
vi. Sheria ya Mtoto, 2011.
b. Machapisho katika Gazeti Rasmi la Serikali
i. The High court Holidays Rules;
ii. Kanuni za Jeshi la Kujenga Uchumi za 2010;
iii. Kanuni za Kura ya Maoni za Mwaka 2010;
iv. Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2010;
v. The Students Regulations 2010 (Journalism and Mass Media College);
vi. Kanuni za Uchaguzi 2010;
vii. The Copyright Licensing of Public Performance and Broadcasting Regulations, 2009; na
viii. The Zanzibar. Municipal Council (Control of Animals and Poultry) By Laws, 2010.

Kiambatanisho 8a: Vizazi na Vifo vilivyosajiliwa kiwilaya

Wilaya	Vizazi			Vifo		
	wanawake	wanaume	Jumla	wanawake	wanaume	Jumla
Mjini	7632	7,529	14,370	205	323	528
Magharibi	1,379	1,416	2,795	39	52	91
Kaskazini A	651	909	1,560	35	52	87
Kaskazini B	564	712	1,276	20	27	47
Kusini	274	347	621	25	30	55
Kati	182	215	397	12	23	35
<i>Jumla Unguja</i>	4682	11,128	21,019	336	507	843
Wete	1,889	2,518	4,407	69	97	166
Micheweni	1,495	1,624	3,119	73	88	161
Chakechake	1,999	2,451	4,450	81	86	169
Mkoani	1590	1700	3,290	67	119	186
<i>Jumla Pemba</i>	6,973	8,293	15,266	290	390	679
JUMLA KUU	11,655	19,421	36,285	626	897	1,523


Kiambatanisho 8b: Nyaraka zilizosajiliwa

AINA YA NYARAKA	IDADI YA USAJILI
A-1 (AMANA)	19
A-2 (MAUZO/URITHI)	178
A-3 (WAKFU,HIBA, KIAPO, UHAULISHAJI VYOMBO VYA MOTO)	557
A-4 (KUFUTA AMANA)	5
JUMLA	756

Kiambatanisho 8c: Usajili wa Kazi za Hakimiliki

AINA YA KAZI	2007/2008	2008/2009	2009/2010	2010/2011
Miziki	318	50	103	10
Qasida	5	16	5	8
Vitabu	13	11	2	5
Filamu	1	6	3	5
Mawaidha	0	0	0	26
Miswada ya Vitabu	30	15	15	5
Miswada ya Filamu	0	0	5	3
Tamthiliya	15	1	8	1
Maandishi ya Miradi	0	0	1	1
Michoro	0	22	0	1
JUMLA	382	121	137	64

Chati 1



Kiambatanisho 9: Vikundi vilivyosafirisha Mahujaji 2010

a) Ahlu Daawa Hajj and Travelling Agency	114
b) Alfirdaus	99
c) Alharamayn Development Fund	131
h) Al-Maarifa Charitable Centre	70
d) Hajj Caravan	100
e) Jumuiya ya Istiqama	229
f) Khidmat Islamiyya Charitble Society	131
g) Zanzibar Hajj and Travelling Agency	80
i) Zanzibar Istiqama Hajj and Travelling Agency	187
Jumla	1141

Kiambatanisho 10a: Idadi ya Wafanyakazi 2010/2011

Idara/Taasisi	Jumla	Unguja		Pemba		Wafanyakazi Kielimu		
		W/me	W/ke	W/me	W/ke	Cheti au chini	Stashahada au zaidi	% Stashahada au zaidi
Mahkama	299	138	64	67	30	239	60	20%
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	39	24	15	0	0	23	16	41%
Tume ya Kurekebisha Sheria	7	5	2	0	0	2	5	71%
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	74	38	21	11	4	36	38	51%
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	8	4	4	0	0	2	6	82%
Idara ya Utumishi na Uendeshaji	51	31	20	0	0	36	15	30%
Afisi Kuu Pemba	37	0	0	21	16	28	9	24%
Idara ya Mufti wa Zanzibar	39	18	11	8	2	28	11	28%
Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali	71	35	21	10	5	47	24	34%
Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	6	0	5	1	0	0	6	100%
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	95	40	20	24	11	77	18	19%
Jumla	726	333	183	142	68	518	208	29%

Kiambatanisho 10b: Wafanyakazi Waliopo Mafunzoni 2010/2011

IDARA	SHAHADA YA UZAMILI		STASHAHADA YA UZAMILI		SHAHADA YA KWANZA		STASHAHADA YA JUU		STASHAHADA		CHETI		JUMLA
	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	KE	ME	
Mahkama		2							1	4	2	3	12
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	3	1								1			5
Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka		1				1			2	2	1	1	8
Tume ya Kurekebisha Sheria	1	1											2
Idara ya Mipango na Sera		1			1								2
Idara ya Utumishi na Uendeshaji													
Afisi Kuu Pemba					1	1			2	2	1		7
Afisi ya Mufti wa Zanzibar									1		2	1	4
Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali					1				1	1		1	4
Afisi ya Msajili wa Hakimiliki		1											1
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana		2			1	2				2	2		9
JUMLA	4	9			4	4			7	12	8	6	54

Kiambatanisho 10c: Wafanyakazi Waliopatiwa Mafunzo ya Muda Mfupi 2010/2011

NA	IDARA/TAASISI	W/KE	W/ME	JUMLA
1	Mahkama	30	18	38
2	Afisi ya Mwanasheria Mkuu	1	1	2
3	Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	0	0	0
4	Tume ya Kurekebisha Sheria	1	3	4
5	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	0	0	0
6	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	0	0	0
7	Afisi Kuu Pemba	0	0	0
8	Afisi ya Mufti wa Zanzibar	0	0	0
9	Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali	0	0	0
10	Afisi ya Msajili wa Hakimiliki	2	0	2
11	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	0	0	0
	JUMLA	34	22	46